


# MIUNGANISHO

**Wahitimu wa Classical High School** Usiku wa Jumatatu katika Veterans Memorial Auditorium. Hongera Wahitimu!

## KONA YA AFISA MKUU MSIMAMIZI

JUNI 14, 2023



DKT. JAVIER MONTAÑEZ
AFISA MKUU MSIMAMIZI

Tukiwa na chini ya wiki mbili kukamilisha mwaka wa shule, nataka kushiriki jinsi najivunia kwa kila mwanafunzi wetu ambaye alifika katika hatua ya mwisho. Wiki za mwisho za shule zimejazwa na usafiri uwanjani wa mwisho wa mwaka, karamu na sherehe za kuhitimu. Daima inafurahisha kutazama furaha katika macho ya wanafunzi wetu wakati wanajitayarisha kwa majira ya joto.

Kwa wahitimu wetu wote wa shule za sekondari, hongera! Kuna njia nyingi na maisha ni kuhusu uchaguzi unao fanya. Kuwa na imani, jiamini, waza kwa busara, pata kikundi cha kukusaidia, na daima jiulize 'itakuwaje?' Tazama ujumbe kwa nyinyi nyote hapa kutoka kwa anwani yangu ya masika kwa wanafunzi katika Brown Day.

Tunafurahia kuzindua **Mpango wa Masomo ya Majira ya Joto** mnamo Julai 10! Mpango wa Masomo ya Majira ya Joto utafanyika Julai tarehe 10 hadi Agosti tarehe 17. Bada kuna nafasi katika mpango kabambe wa middle school ambao ume jazwa na fursa bora ikiwemo Mpango wa Majira ya Joto SeaPerch pamoja na mtaala wa robotiki wa STEM ambao uta malizia kwa mashindano ya uundaji wa boti. Pia kuna E-michezo, Michezo ya Kieletroniki, mpango ambapo wanafunzi wanatumia michezo ya video ya wachezaji wengi kutengeneza mazingira yakujumishwa na yenye usawa ambapo wanafunzi wote wanaweza kufanikiwa. Jisajili hapa ikiwa unapendelea.

Wanafunzi wengi wa shule za sekondari wamepokea barua ziki pendekeza kwamba wajiunge nasi katika mpango huu wa masomo ya majira ya joto. Mpango huu utatumia jukwaa la mtandaoni la Edgenuity na kuchanganya masomo mtandaoni pamoja na mafundisho ya mwalimu, kazi za vikundi na miradi. Mpango wa shule ya sekondari ni mpango wa marudio unaofanya kazi kusaidia wanafunzi wafikie mahitaji yao ya kuhitimu. Pia tuko na mpango kabambe wa CTE wa majira ya joto kwa shule za sekondari.

Tuko na zaidi ya wanafunzi 1 200 waliosajili katika Akademia ya Masomo ya Majira ya Joto ya Stars. Bado tunapokea majina katika mpango huu katika orodha ya shule hii ya chekechea hadi darasa la 5. Mpango huu wa majira ya joto utajumuisha mtaala wa kusoma na kuandika na hisabati pamoja na kipengele kabambe cha hisia kijamii.

Ikiwa wewe au mtu unayemjua atakosa mojawapo ya vijarida vyetu, unaweza kupata matoleo ya awali kwenye tovuti ya Wilaya katika lugha nyingi.

# TAARIFA MPYA ZA WILAYA



## RI HOTUBA YA HALI YA ELIMU

Hivi majuzi, wakati wa hotuba yake ya Hali ya Elimu katika Shule ya Viziwi ya Rhode Island, **Kamishna Angélica Infante-Green** aliangazia uboreshaji kadhaa katika matokeo kwa Surveyworks katika kuridhika kwa wazazi, wanafunzi na walimu. "Kupitia uingiliaji kati huu, tuna vunja matarajio ya kale na kujenga mapya, hatua kwa hatua!" alisema Infante-Green. Data ya Surveyworks inaonyesha kwamba wanafunzi wanaongea zaidi kuhusu chuo na taaluma. Wanafunzi wanatumia zaidi mipango ya kusoma kibinafsi na wanadhani hii ina umuhimu. Zaidi na hayo, utafiti unaonyesha kwamba walimu wamefurahishwa na mtaala na kuna mtazamo chanya katika uongozi wa Wilaya na usalama. Tumeona ongezeko la 5-9% katika sehemu hizi. Na mwishowe, kwa majibu ya **ushirikiano wa familia** , Surveyworks imeonyesha **ongezeko la 9% kwa kupendwa ambayo ni 5% zaidi kuliko wastani ya jimbo**. Kazi bora kutoka kwa wafanyakazi wetu wote, familia na wanafunzi. Asante kwa kuchukua muda kukamilisha utafiti. Tumefurahia matokeo.

## MPANGO WA VITABU VYA KIELIMU

Mnamo Ijumaa, **Asa Messer Elementary School** ita andaa siku ya kitabu kusherekea mafanikio ya wanafunzi na kusaidia kuanzisha bidii za masomo ya majira ya joto. Katika tukio hilo, wanafunzi 60 wa darasa la pili na wa darasa la tatu watashiriki katika shughuli za uwanjani na kupokea vitabu vya Elimu vinavyo lingana na umri wao kuongezea katika maktaba zao za nyumbani.

Utafiti unaonyesha kwamba njia moja ya kudumu na ambayo ina ambatana pakubwa na alama za kusoma ni idadi ya vitabu nyumbani. Usambazaji wa vitabu katika tukio ni kumalizia kwa mpango mkubwa wa wilaya wa K-5 kujenga maktaba za nyumbani. Katika wiki mbili zijazo, Wilaya ya Shule ya Umma ya Providence ita sambaza vitabu 90, 000 vinavyo ambatana na umri na wanafunzi wote wa K-5 wakipokea vitabu 10 na begi la Shule za Providence. Kulingana na Mwalimu wa Masomo na Ripoti ya Mwalimu Mkuu, walimu wengi (96%), walimu wakuu na wasimamizi wa maktaba wa shule wanasema kwamba kuwezesha ufikiaji kwa vitabu nyumbani kwa mwaka mzima ni muhimu kuboresha mafanikio ya mwanafunzi.

"Mpango huu umeundwa kusaidia watoto wetu wapate ujuzi unaohitajika kufaulu ndani na nje ya shule, na wakati sawia kujenga mazingira ambapo wanafunzi wote wa Shule ya Umma ya Wilaya ya Providence wapate upendo na shauku katika kusoma," alieleza **Kamishina Angélica Infante-Green** & **Afisa mkuu msimamizi Javier Montañez** katika barua kwa familia kuhusu **mpango wa "Vitabu vyangu Majira ya Joto"**.

## PCTA INAKAMILISHA DIPLOMA KWA WILAYA

Wanafunzi na wafanyakazi katika **Akademia ya Taaluma na Ufundi ya Providence** ilifanya kazi na usimamizi na wafanyakazi wa shule kutengeneza diploma kwa wahitimu wote wa shule za sekondari. Hongera kwa **Graham Walker** wa PCTA na wanafunzi wake kwa kuvuka mstari wa mwisho wiki hii wakati walipo chapisha tena vyeti kidogo vya dakika ya mwisho. Huu ni mwaka wa tatu wanafunzi na wafanyakazi wamefanya kazi pamoja kukamilisha hizi kwa undani. Hapo zamani, diploma zilichapishwa na mtoa huduma wa nje. Ni uzoefu bora wa masomo kwa wanafunzi kabla ya kuhitimu.



## SIKU YA KUREMBESHA YA MOUNT PLEASANT



Wanafunzi na wafanyakazi katika **Mount Pleasant High School** walifanya kazi kwa bidii Jumamosi hii iliyopita kusaidia kurembesha uwanja wa shule kwa kupanda maua mbele ya shule. Shukrani maalum kwa Mwalimu mkuu wa Mount Pleasant Wobberson Torchon kwa kusaidia kupanga hii siku bora kwa wanafunzi wetu na wafanyakazi wetu.




# USAWA NA USHIRIKI

*Ofisi ya Usawa na Ushiriki unatambua mwezi wa Juni kama mwezi wa kutafakari, uhuru, heshima, usawa, ushiriki na upendo. Kama una sherekea Juni tarehe kumi au PRIDE au zote, tuna kuuliza kwamba ukumbuke wote walio jitolea mhanga kuhakikisha tunaweza kuendelea kutetea kwa ujasiri, kwa uhuru na nafasi ya vita vya ukombozi, haki na haki kuwa binafsi zetu aili.*

**RESPECT Akademia ya Uongozi**

**Jumatatu, Agosti 14, 2023 - Ijumaa, Agosti 25, 2023**

**Eneo:** Chuo kikuu cha Brown

**Hadhira:** Wanafunzi wa PPSD Middle & High School

*Bila malipo kwa wanafunzi ambao wamekuwa washiriki amilifu katika RESPECT. Kiamsha kinywa, chakula cha mchana na vitafunio vitatolewa. Wanafunzi watapata posho. Jisajili hapa.*

**Mkutano wa emPOWER kwa Walimu wa Rangi**

*Usisahau kusajili mwezi huu kwa mkutano wa emPOWER unao andaliwa mnamo Juni 20, 2023 saa kumi unusu jioni 4:30pm katika Bom Bom Nutrition (375 Washington St. Providence, RI 02903). Jisajili hapa! Tunatumaini kukuona hapo! Ikiwa una maswali yeyote, tafadhali wasiliana nasi katika equity@ppsd.org. Walimu wote wa PPSD wanakaribishwa kuhudhuria.*

**Ofisi ya Central Chakula cha mchana na Masomo: Kujifunza kuhusu Muktadha na Historia ya Juni tarehe kumi**

*Mwaka huu, mada ya Juni tarehe kumi ni "Wimbi la Uhuru". Mnamo Alhamisi Juni 15, 2023 kuanzia saa sita mchana hadi saa saba na robo mchana 12:00-1:15pm kuja ujifunze na Ofisi ya Usawa na Ushiriki kuhusu muktadha na historia ya Juni tarehe kumi. Juni tarehe kumi ni makumbusho ya sherehe ya kitaifa ya kale sana kuhusu kusitishwa kwa utumwa huko Marekani. Juni tarehe kumi ina sherekea urithi wa uhuru na ukinzani wa kizazi cha watu Waafrika na wale ambao walikuwa watumwa awali. Ikiwa ungependa kujifunza na kujadili zaidi kuhusu hii historia kabambe tafadhali jiunge nasi katika chumba cha bodi ya shule pamoja na chakula chako cha mchana na marafiki zako! Tazama hizi shughuli kwa kazi, nyumbani na shule.*

**Juni tarehe kumi na Sherehe ya Mwezi wa Majivuno Nafasi ya Ubunifu**

*Kwa heshima ya LGBTQ+ mwezi wa Majivuno na Juni tarehe kumi, ofisi yetu ina andaa nafasi ya ubunifu kusherekea vijana na mashirika yetu yanayo hudumia vijana! Jioni hii itajumuisha chakula, muziki , sanaa na ufundi. Tukio hili litafanyika mnamo Juni tarehe 15, 2023, kuanzia saa kumi na moja jioni hadi saa moja usiku 5pm-7pm katika 797 Westminster St katika Chumba cha PD Tech (Ghorofa ya chini) . Mada ya tukio hili ina angazia kujenga muungano wa kijamii na kuunga mkono usemi wa usanii. Kama unajitayarisha kwa tukio linalo husiana na majivuno, tukio la Juni tarehe kumi, au ungependelea tu kupumzika kwa kutengeneza bangili, tuna peana nafasi na uwezo wa kufanya hivyo.*

## WEKA ALAMA KWENYE KALENDA ZENU!

- **JUNI TAREHE KUMI (HAKUNA SHULE)**
  Jumatatu, Juni 19
- **SIKU YA MWISHO SHULE**
  Ijumaa, Juni 23
- **MPANGO WA MASOMO YA MAJIRA YA JOTO**
  Jumatatu, Juni 10 - Alhamisi, Agosti 17

## JUNI MENYU YA SHULE



# KUWASHEREHEKEA WANAFUNZI

Wanafunzi wetu wenye bidii na wenye talanta wanafanya mambo mazuri kila siku. Hapa kuna mifano michache.



## WANAFUNZI WA CENTRAL WANABUNIFU NEMBO MPYA YA MLL

Hongera kwa mwanafunzi wa **Central High School** Rosalinda ambaye alipokea tuzo kwa kazi yake ya ubunifu katika nembo mpya ya PPSD ya MLL (Mwanafunzi wa Lugha Nyingi)! Asante kwa kila mtu ambaye aliwasilisha muundo wa nembo mpya, tuli pokea ubunifu nyingi nzuri kuchagua. Hongera kwa kazi yako ya bidii, Rosalinda!



## PPSD WANAFUNZI BORA WA KWANZA NA WA PILI

Hongera kwa wanafunzi wetu wakubwa wanao hitimu, lakini pongezi maalum kwa **Wanafunzi bora wa kwanza na wa pili wa PPSD** wa mwaka wa 2023! Wanafunzi wamepata fursa ya kukutana na **Meya Brett Smiley**, na hata pia washirika kutoka Kamati ya Jiji la Providence, kusaidia kusherekea mafanikio yao. Tunangojea kwa hamu kutazama wahitimu wetu wote wakati wa sherehe!




## CTE SIKU YA KUTIA SAINI

Hongera kwa wanafunzi 84 wa PPSD ambao wamepokea taaluma kutoka kufundishwa kazi/muugano, na nafasi za muda wa kuduma katika viwanda. Walisherekewa wiki iliyopita wakati wa Siku ya Kutia Saini katika **Providence Career & Technical Academy (PCTA)**. Kampuni na viwanda kumi na nne walijiunga na tukio ambapo wanafunzi "walitia saini" kwa waajiri wao wa baadaye ambayo ili jumuisha Electric Boat, Building Futures, LiUNA, RI Women in the Trades, Navarrete Tire Shop, Bristol Toyota, 401 Automotive, Carpenters Union, Jutras Woodworking, JD Cementworks, Providence Parks & Recreation, Lucia's Mexican Restaurant na Mkahawa wa Waterman Grille.



## WANAFUNZI WA BAILEY WANAMETAMETA

Wanafunzi kutuka **Robert Bailey Elementary School** walifanya maonyesho kutoka Disney "Kitabu cha Mwituni cha Watoto" wakati wa maonyesho katika Kituo cha Maonyesho ya Sanaa cha Providence (PPAC) hii wiki iliyopita! Bailey Elementary ilikuwa mmoja wapo wa Shule nne za Rhode Island zilizofanya maonyesho katika Muziki za Disney Shuleni' "Yote Inaanza kwa Ndoto," Kazi nzuri sana kutoka kwa kila mtu!



## RUFAA YA KUIGA

Wanafunzi kutoka **Nathan Bishop Middle School**washiriki katika Rufaa ya Kuiga katika Mahakama ya Providence Federal. Kutambua Haki ili shirikiana na Nathan Bisho kusaidia wanafunzi kujifunza zaidi kuhusu sheria na haki. Shukrani kwa Mahakimu Waheshimiwa wote kwa kujitolea muda wao kuongea na wanafunzi!




## RHODE ISLAND SIKU YA URAIA

Hongera kwa wanafunzi wetu wote wa PPSD ambao walifanya maonyesho katika Siku ya Uraia katika Rhode Island kwa Manispaa na Ikulu ya Serikali! Pongezi maalum kwa wanafunzi wa **E-Cubed Academy** kwa kushinda Tuzo la Utendaji, mwanafunzi wa **360 High School** kwa kushinda Tuzo la Mwanafunzi wa Kuleta Mabadiliko, na wanafunzi wa **Hope High School** ambao walishinda Tuzo la Ushirikiano na Utofauti!

# NI HABARI NJEMA: PPSD KWENYE VYOMBO VYA HABARI

- Hawa wanafunzi walikuwa hawafanyi vyema wakati wa janga. Halafu mshauri wa mwelekezo akawapatia usaidizi
  Jarida la Providence, Juni 7, 2023
- Wanafunzi wakale wa Patriots wana tembelea shule ya Providence kutuza wanafunzi kwa kuboresha mahudhurio
  WJAR, Juni 1, 2023





# KUANGAZIWA KWA MWANAFUNZI

**Wajue wanafunzi wetu hodari wa darasa la juu Wilayani!**

**Jonas Genao**
*Mwanafunzi mkubwa, Alvarez High School*
ES: Jamhuri ya Dominika
MS: Roger Williams

**Ismerai Nunez**
*Mwanafunzi mkubwa, Alvarez High School*
ES + MS:
Union City, NJ

***Mipango yako ni gani baada ya shule ya sekondari?***

**KATIKA:** Napanga kwenda kwa chuo kwa miaka 4-URI. Nimechagua URI, kifedha, ilikuwa uchaguzi bora kwangu. Nimependezwa na mpango wao wa haki ya jinai na saikolojia. Katika umri mdogo, nili pitia vurugu kali na mtu aliye karibu nami. Nilikuwa hapo na kulikuwa na mkasa. Baada ya hapo, sikutaka mtu yeyote apitie uzoefu wangu. Sijui kazi maalum nataka kufanya lakini nataka kusaidia watu na kusaidia kuzuia mikasa kama hii.

Niliwasilisha ombi kupitia URI na Mpango wa Ukuzaji wa Talanta. Ukuzaji wa Talanta una ajiri na kuhudumia wahitimu wa shule za Rhode Island wenye uwezekano wa chuo ambao wanatoka mazingira ya changamoto kihistoria, wengi wao wakiwa Wanafunzi wa rangi. Lengo la mpango ni ufikiaji, fursa, bei nafuu na ukamilishaji.

> **“Naweza kusema profesa nilio kuwa nao walinisukuma kufanya bora zaidi na kujaribu uwezo wangu wote. Napenda kupewa changamoto.”**

**JG:** Mwaka ujao, nitaenda URI na kufuatilia masomo ya sayansi ya kompyuta. Ilibidi niwaze katika shule mbili na nikawaza mpango wa URI wa Ukuzaji wa Talanta utakuwa bora. Pia nilitazama Taasisi ya Chuo cha Ufundi cha Worcester na Chuo kikuu cha Clark. Nitaishi katika URI mwaka wa kwanza kama inavyo hitajika na mpango. Pia, shule haiko mbali kutoka nyumbani kwangu, kutoka familia yangu.

Napendelea ubunifu ambao unaweza kutekeleza katika sayansi ya kompyuta. Napenda hisabati. Chochote ambacho unaweza kuongezea hisabati, napenda. Unaweza kutengeneza vitu vingi kupitia sayansi ya kompyuta. Vitu muhimu na pia inafurahisha. Iko na uwezo mkubwa wa ubunifu ndani yake.

***Kwa nini ulichagua Alvarez?***

**KATIKA:** Sikuwa najua kuna uchaguzi wa shule wakati nilipokuwa na anza. Nilikuja wakati wa COVID. Nilifanya majaribio na wakaniweka hapo. Nimekutana na watu wazuri. Nimekuwa na profesa wazuri.

Naweza kusema profesa nilio kuwa nao walinisukuma kufanya bora zaidi na kujaribu uwezo wangu wote. Napenda kupewa changamoto. Sipendi kuchukua njia rahisi.

**JG:** Nachagua Alvarez kwa sababu ya umbali. Nilikuwa mgeni nchini. Nilikuja hapa katika darasa la 8 kutoka Jamhuri ya Dominika. Ilikuwa karibu na nyumba yangu kwa hivyo nilichagua Alvarez.  Uzoefu wetu umekuwa na changamoto. Kwa hakika kuwa mgeni nchini kila kitu kilikuwa tofauti. Mwaka wangu wa kwanza ulikuwa mzuri lakini COVID ilikuja na mambo yakaanza kuharibika. Sijashiriki katika shughuli nyingi za mtaala wa ziada. Lakini nimejihusisha katika madarasa ya ukuzaji wa taaluma kama sayansi ya kompyuta na kufanya madarasa mengi ya AP. Pia nje ya shule, nilifanya mpango wa ukuzaji wa uongozi, HOBEY. Nilifanya Akili Bandia katika kambi ya mazoezi pamoja na Mark Cuban. Ilikuwa mtandaoni.

***Je, kuna mwalimu aliyekuwa na athari kubwa kwako?***

**KATIKA:** Bwana Chandley, na mwona hapa kila mara. Yeye ni profesa wa kompyuta. Mimi siko bora sana kwa kompyuta lakini alifanya darasa liwe la kufurahisha. Alifanya iwezekane kwa mwaka wangu wa mwisho kuchukua darasa lingine naye. Alinisaidia. Tulikuwa na wakati mzuri.

**JG:** Bwana Chandley, mwalimu wangu wa sayansi ya kompyuta. Amekuwa mshauri wangu katika Sayansi ya Kompyuta. Tumeanza kusoma na tume jadili sana mada nyingi katika sayansi ya kompyuta na hata pia mada ya nje kama vitabu na kadhalika. Amekuwa kama rafiki wangu wa dhati wakati nilipokuwa hapa.

***Uzoefu ninao kumbuka zaidi?***

**KATIKA:** Dansi ya kuhitimu mwaka uliopita na mwaka huu. Naenda mwaka huu na kikundi cha wanafunzi wa CCRI.

***pg. 6, kuendelea kwa Kuangaziwa kwa mwanafunzi***

Nikama nimemaliza shule ya sekondari na nafanya mwaka wangu ulio baki pamoja na wanafunzi wa Alvarez na CCRI. Mpango wote ulitufanya tuwe na uhusiano bora.

Muhula wangu wa kwanza CCRI, nilifanya masomo yangu ya msingi ambayo nilihitaji kuhitimu. Muhula wangu wa pili, nilifanya masomo ya utaalamu wangu. Kwa hivyo nilichukua utaratibu wa jinai, uhalifu na saikolojia ya jumla. Pia nilifanya darasa la nne kupitia mtandaoni. Nikifaulu masomo, napata alama kamili za chuo. Kwa hivyo, nikianza URI nitaanza na alama 24. Labda nitahitaji miaka 3 kuhitimu sasa. Kwa vile nataka kupata shahada ya pili, labda itachukua miaka zaidi.

**JG:** Nilipata 2 katika jaribio langu la AP Sayansi ya Kompyuta. Na siku hiyo, sikuwa nahisi vyema na nilijitayarisha vizuri lakini bado nilihisi vibaya. Halafu nikaona matokeo na nilipata alama ya kufaulu.

***Una wasiwasi au una shauku gani kwa kuhitimu?***

***KATIKA:*** Sasa hivi, nina wasiwasi kuhitimu kwa sababu mimi ni mwanafunzi bora zaidi na nilazima nitoe hotuba. Mimi si yule mtu anaye ongea sana kwa umma. Lakini kama lazima nifanye, nitafanya. Ni jukumu langu. Baada ya kuhitimu, nina wasiwasi kuhusu maisha. Nitakuwa naishi chuoni na najua kwamba nina wazazi wangu hapa ambao watani saidia. Lakini nataka kujaribu vitu njia yangu na kuona uwezo wangu ni gani. Nina wasiwasi na msisimko ambao uko mbele yangu.

JG: Nina msisimko wa kuanza chuo kikuu. Nataka kukutana na watu zaidi. Nina msisimko kuanza maisha yangu ya kitaaluma. Sina woga. Nahisi nimetulia na nina msisimko

# WILAYANI




## YEAW AMETAJWA KUWA MSIMAMIZI WA MAKTABA WA MWAKA

Hongera kwa **Kimberly Yeaw wa Akademia ya Taaluma na Ufundi ya Providence** ambaye alitajwa kuwa Msimamizi wa Maktaba wa Mwaka kupitia Wasimamizi wa Maktaba wa Shule wa Rhode Island! Hizi ni baadhi ya sababu Bi. Yeaw ni wa kipekee:

1. Anafika mapema kila siku ili wanafunzi wawe na nafasi kimya ya kupumzika wakati wa asubuhi.
2. Anafungua maktaba yake wakati wa chakula cha mchana ili wanafunzi waweze kula chakula cha mchana kwa mpangilio wa buhari.
3. Anabaki na usasisho wa mtindo wa usomaji na anajaza maktaba yake kwa kuzingatia mtindo huo.
4. Daima ofisi yake iko wazi kwa wanafunzi ambao wanahitaji nafasi kuchakata na kuwaza. (Walimu pia!)
5. Kama mkufunzi wa kale wa PAR, Kim daima anapatikana kusoma SLO ya walimu, au kusaidia kuhesabu data.
6. Kim amepanga nafasi yake kupatia PCTA kituo cha usaidizi kwa teknolojia.
7. Anafanya kazi na Kikundi cha Dell Tech cha shule yetu na anasaidia wanafunzi kudhibiti masomo yao.
8. Kim ni wa kwanza kujitolea kwa matukio ya wanafunzi, au kusaidia kupanga mipangilio shule nzima.



## MKUTANO WA VIONGOZI WA JUMUIYA

Zaidi ya washiriki 40 wa jumuiya walijiunga na Carina Pinto de Chacon, Chifu wa **Ushirikiano wa Familia na Jumuiya**, hivi majuzi kwa Mkutano wa Viongozi wa Jumuiya katika United Way ya Rhode Island huko Providence. Timu ili jadili umuhimu wa mahudhurio na ukamilisho wa FAFSA kwa wanafunzi wetu na pia mpango unao kuja wa masomo ya majira ya joto. Shukrani kwa wote walio jiunga nasi!




## WANAFUNZI WA DARASA LA SANA WANA TEMBELEA SHULE ZA SEKONDARI

Wanafunzi wa darasa la saba kutoka **PPSD Esek Hopkins Middle School** walikaribishwa kwa shule za sekondari za Wilaya katika wiki zilizopita. Wanafunzi wa middle school wa Wilaya walipata fursa kutembelea shule, kukutana na walimu na kusaidia kutathmini mapendeleo yao kabla ya kuingia katika mchakato wa uchaguzi wa shule mwaka ujao.



## MARTA APARICIO ANATEMBELEA CENTRAL

Wanafunzi katika **Central High School** walikaribisha Hope High School 2010 Idara ya Jimbo ya Mwanafunzi bora Mwanadiplomasia **Marta Aparicio**, pamoja na Meya wa Providence Brett Smiley, kujifunza kuhusu taaluma yake ya kidiplomasia kimataifa. Wanafunzi walivutiwa kwa hadithi yake ya ajabu. Asante kwa kutembelea, Marta!



## MFUNGANO MAALUM WA OLIMPIKI

Hongera kwa mkaazi wa Rhode Island Brian Johnson ambaye atawakalisha Jimbo la Ocean katika Olimpiki Maalum akicheza bocce! Ndugu wa Brian, Dan Johnson, ni mwalimu katika **A-Venture**, na walikuwa na sherehe ya kwa heri kwa Brian! Bahati njema kwa Brian na timu yote ya Marekani ya Olimpiki Maalum!



## MAONYESHO YA LUGHA MBILI NA KUFAHAMU LUGHA MBILI

Viongozi wa elimu walijiunga nasi wakati wa Shule za Umma za Providence **Maonyesho ya Lugha Mbili na Kufahamu Lugha Mbili** kutazama mpango ukitendeka na hata pia kuongea na wanafunzi na walimu kuhusu uzoefu wao. Timu ili tembelea madarasa katika **Alfred Lima**, **Lugha Mbili Leviton** na **Lillian Feinstein katika Sackett Street Elementary Schools**. Shukrani maalum kwa Engage2Learn (e2L) kwa kusaidia kuandaa tukio hilo. Kwa ushirikiano na e2L, viongozi wa Wilaya na washika dau wamekuwa wakifanya kazi kutengeneza mpango wa mafunzo na ukuaji uliotengenezwa kuwezesha walimu kusaidia kwa usawa ELLs.

Providence Schools

© 2023 Providence Public Schools · communications@ppsd.org · www.providenceschools.org

Mambo ya kusisimua yanatokea katika Wilaya nzima na tunataka kueneza ujumbe! Ikiwa una programu, hafla, Mfanyakazi au mwanafunzi mwenye hadithi nzuri ajabu ambayo ungependa kuonyesha, tafadhali tuma barua pepe kwa communications@ppsd.org.